ANSAF
Agricultural Non State Actors Forum

# MIKOPO YA 10% YA HALMASHAURI ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MAKUNDI YA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.



JUNI, 2024

info@ansaf.or.tz

www.ansaf.or.tz



# UTANGULIZI

Mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa vijana wanawake na watu wenye ulemavu inafanya kazi kama mfuko unaozunguka ambapo Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura ya 290, Kifungu cha 37a) inazielekeza Halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya kila mwaka kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake (4%), vijana (4%) na watu wenye ulemavu (2%). Mikopo hii inakusudiwa kuimarisha shughuli zinazowaingizia kipato wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wasio na ajira rasmi na hivyo kuboresha maisha yao kwa ujumla.

Utoaji wa mikopo hii ulisitishwa na Waziri Mkuu, Mhe. Majaliwa Kassim, Aprili 2023 kwa maelekezo ya Rais, baada ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kufichua mapungufu katika usimamizi wa mikopo hii.

**Mapungufu yaliyoainishwa ni pamoja na:**

- Halmashauri 53 kutotenga shilingi bilioni 5.06 kutoka asilimia 10 ya mapato yao kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kinyume na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.
- Halmashauri 180 kushindwa kukusanya marejesho ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 88.42 katika (kati ya hizo halmashauri 9 zilitoa shilingi bilioni 2.25 zilitolewa kwa vikundi 627 vilivyoacha shughuli za biashara) kutokana na upungufu wa uwezo wa maafisa maendeleo ya jamii wa kutathmini, kusimamia, kufuatilia na kutoa mafunzo kwa vikundi vya wanufaika wa mikopo.
- Halmashauri 9 kutoa shilingi bilioni 2.25 billion kwa vikundi 627 ambavyo havifanyi tena biashara.
- Halmashauri 3 kutoa shilingi bilioni 895.94 kwa vikundi 48 ambavyo havipo.
- Vikundi 201 vya wanufaika wa mikopo katika Halmashauri 8 kutumia vibaya shilingi milioni 774.66 zilizotolewa kama mikopo na kuzisambaza kwa wanavikundi badala ya kufadhili miradi ya biashara iliyoidhinishwa.

*“ Mikopo ya 10% ya Halmashauri za Serikali za Mitaa inakusudiwa kuimarisha shughuli zinazowaingizia kipato wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wasio na ajira rasmi.”*

- Halmashauri 45 kutoa mikopo ya shilingi bilioni 20.79 bila kuzingatia uwiano wa utoaji wa mikopo wa 4% kwa wanawake, 4% kwa vijana na 2% kwa watu wenye ulemavu,
- Halmashauri 1 kutoa mikopo ya milioni 147.26 kwa vikundi 5 vyenye watu walioajiriwa rasmi kinyume na kanuni ya 6(1)(f)y ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo,
- Kushindwa kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa vikundi vya wanufaika wa mikopo katika ngazi ya kata, na
- Kutohusihwa kwa wataalam wa usimamizi wa mikopo katika mchakato wa utoaji na urejeshaji wa mkopo na kusababisha ongezeko la mikopo chechefu.




Changamoto kama hizo pia zilijitokeza katika utafiti uliofanywa na ANSAF mwaka 2019 ili kutathmini uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 kwa ajili ya mikopo hii katika wilaya 25 nchini Tanzania. ANSAF pia iliona changamoto hizo katika utekelezaji wa mradi wa "Kuimarisha usimamizi na utawala wa mfuko wa uwezeshaji wanawake, vijana na watu wenye ulemavu" katika wilaya 25 hizo uliokuwa ukifadhiliwa na Ubalozi wa Finland Tanzania.




Kufuatia kusimamishwa kwa mikopo hii, ANSAF ilifanya utafiti kwa njia ya mtandao na mkutano wa mashauriano ngazi ya kitaifa kwa kushirikiana na MEDA Tanzania. Lengo lilikuwa ni kuwaleta pamoja wanawake, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na asasi za kiraia zinazoongozwa na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ili kujadili namna bora ya usimamizi wa mikopo hii na kutoa mapendekezo kwa ajili ya kuongeza ufanisi na utendaji wa mikopo.

[1] Halmashauri hizi ni Nyamagana, Sengerema, Musoma Vijijini, Bukoba Mjini, Karagwe, Muleba, Bukombe, Bariadi, Karatu, Longido, Monduli, Korogwe, Babati, Mvomero, Ulanga, Kilosa, Kilwa, Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala, Rungwe, Njombe, Iringa Vijijini, Mufindi na Momba.

Matokeo ya utafiti wa mtandaoni kuhusu utoaji wa mikopo ni kama ifuatavyo:




Mapendekezo ambayo yaliyokusanywa yaliwasilishwa kwa kamati ya kitaifa ya maboresho ya mfumo wa utoaji mikopo ambayo ilikuwa imechaguliwa na waziri wa TAMISEMI. Mapendekezo hay oni pamoja na:

1. Kuanzisha mfumo huru wa usimamizi katika kila Halmashauri, kama ilivyo kwa Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali chini ya SIDO. Wanufaika wa mikopo walikua na mashaka ya kwamba utoaji wa mikopo hii kupitia mfumo rasmi wa kibenki hautafanikiwa kufikia malengo ya mikopo hii ya 10% kutokana na vigezo na masharti ya kibenki.

2. Kuwajengea uwezo viongozi wa serikali wanaohusika na usimamizi wa mikopo ili kuimarisha utendaji na ufanisi.

3. Kuweka kipaumbele katika kujengea uwezo vikundi vya wanufaika kabla ya kutoa mikopo.

4. Kuwekeza rasilimali watu na fedha za kutosha. Hii ni pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya usimamizi wa mikopo na kuongeza idadi ya maafisa wa serikali wanaohusika na usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo.

5. Kuruhusu utoaji wa mikopo kwa miradi ya watu binafsi ndani ya vikundi cha wanawake na vijana.



# Urejeshwaji wa Utoaji wa Mikopo ya 10% ya Halmashauri kwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu.



Kwa mujibu wa Waziri wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb), Hotuba ya Bajeti ya 2024/25 utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu utaendelea kuanzia Julai 2024, ambapo:

- Kiasi cha mkopo kinachotarajiwa kutolewa ni shilingi bilioni 227.96, ambapo shilingi bilioni 63.67 ni marejesho yaliyokusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa, shilingi bilioni 63.24 ni asilimia 10 zilizokuwa zikitengwa na Halmashauri wakati utoaji umesimamishwa, na shilingi bilioni 101.05 kiasi kinachokadiriwa kutengwa na Halmashauri kwa mwaka 2024/25.

  Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI inapanga kuendelea kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kukusanya jumla ya shilingi bilioni 43.77 za marejesho kutoka kwa vikundi vya wanufaika wa mikopo.

- Mfumo wa kibenki utatumika kwa Halmashauri 10 za majaribio ambazo ni Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma Ujiji, Songea, Newala, Mbulu, Wilaya za Siha, Nkasi, Itilima, na Bumbuli.

- Halmashauri 174 zilizobaki zitatumia utaratibu ulioboreshwa ambapo kutaanzishwa kitengo cha usimamizi wa mikopo hii OR-TAMISEMI na kamati za usimamizi wa mikopo hii katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, na Kata ili kuondoa mapungufu yaliyosababisha changamoto za awali.

  Majukumu ya kamati za ngazi ya kata ni pamoja na kutambua waombaji, kuhakiki vikundi vya mikopo, na kuvisajili kwenye mfumo kabla ya kuwasilishwa kwenye kamati za Halmashauri.

- TAMISEMI imeanzisha mfumo mpya uitwao Wezesha Portal, ambao utatumika kwa taratibu za utoaji wa mikopo kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mfumo huu utaondoa changamoto za mfumo wa awali kabla ya kusitishwa kwa mikopo.
- Serikali imeajiri maafisa maendeleo ya jamii 787 (ambao wanahusika na usimamizi wa mikopo hii) na kuwapangia kata zilizokuwa na upungufu.



OR-TAMISEMI inapanga:

1. Kuongeza idadi ya wasimamizi wa mikopo katika ngazi ya kata.
2. Kutoa mafunzo kwa watumishi na timu nzima itakayosimamia mikopo hii katika ngazi zote kutoka kwa wataalamu wabobezi wa kusimamia mikopo ya aina hii.
3. Kurekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa inayosimamia mikopo hii na kanuni za utoaji na usimamizi wake ili kuongeza ufanisi.
4. Baada ya kipindi cha mpito, tathmini itafanywa ili kubaini mfumo bora wa utoaji wa mikopo hii

# HITIMISHO

ANSAF inaipongeza Serikali kwa kurejesha utoaji wa mikopo ya 10% ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa vikundi vya Vijana Wanawake na Watu Wenye Ulemavu. Juhudi hizi zinaashiria hatua muhimu katika kurekebisha mapungufu yaliyokuwepo awali na kukuza maendeleo ya kilimo jumuishi. Kwa nia hii, juhudi za kuboresha mifumo, na kujenga uwezo kama ilivyoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya OR-TAMISEMI 2024/25, kuna matumaini ya kuwa na mfumo wa utoaji wa mkopo wenye ufanisi zaidi na matokeo chanya. Utawala na usimamizi bora ni nguzo muhimu katika kuhakikisha kwamba mikopo hii inawawezesha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kukuza ushiriki wao na ustawi katika sekta za kiuchumi.

# MAPENDEKEZO

ANSAF ina mapendekezo yafuatayo:

1. Kwa Walengwa: Kutoa mafunzo endelevu kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu ili kuimarisha uwezo wao katika usimamizi wa fedha, mikopo, na ujuzi wa biashara kwa ajili ya kuboresha utendaji na ufanisi wa mikopo.

2. Kwa Watendaji (Maafisa wa Serikali za Mitaa): Kuwapa mafunzo na kuwajengea uwezo maafisa wa Serikali za Mitaa wenye jukumu la usimamizi wa mikopo ili kuchochea ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo na wanufaika.

3. Kuboresha ufanisi na usimamizi wa mfuko kwa kutenga na kutoa rasilimali za kutosha, kuongeza bajeti ya usimamizi wa mikopo, na kuajiri maafisa wa serikali wa kutosha kusimamia mfuko kwa ufanisi.

4. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga na kutoa asilimia 10 ya mapato ya ndani kwaajili ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na with wenye ulemavu kwa mujibu Sheria ya Serikali za Mitaa, kupitia usimamizi bora na ufuatiliaji.

5. Kukuza uelewa hususan juu ya mahitaji ya sifa za kupata mikopo hii na matumizi ya mfumo wa kidigitali wa Wezesha Portal kwajili ya kufanya maombi ya mikopo kwa walengwa.

6. Kuendelea kutekeleza mkakati bora, jumuishi na shirikishi katika ufuatiliaji na tathmini ya usimamizi na utendaji wa mikopo.

# Hatua Zifuatazo

ANSAF itaendelea kushirikiana na kuunga mkono juhudi za serikali, mashirika yenye nia moja, jamii na wadau wengine muhimu ili kuchangia katika kuimarisha usimamizi na utawala wa mikopo ya asilimia 10 ya Serikali za mitaa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hasa kupitia uhamasishaji, kukuza uelewa na kutoa elimu.

